BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR, KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI.

Mheshimiwa spika, awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru mwenyezi mungu, kwa kutujaalia uhai, afya njema tukaweza kukutana tena katika chombo hiki muhimu cha maamuzi katika nchi yetu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi wa zanzibar.

mheshimiwa spika, vile vile napenda kukushukuru na kukupongeza wewe na wasaidizi wako, mheshimiwa naibu spika na wenyeviti wa baraza kwa uongozi wenu mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha baraza hili ambalo ni muhimili muhimu kati ta mihimili ya nchi . mwenyezi mungu awazidishie hekima na busara ili muweze kutekeleza vyema wajibu wenu katika chombo hiki muhimu cha nchi yetu.

Aidha, naipongeza Wizara kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotupatia Kamati katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawataka wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia hatua na malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawasilisha Ripoti hii kwa mujibu wa Kanuni ya 109(18) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi,Toleo la 2020. Hivyo naomba kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa, Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi imetekeleza sharti hilo la Kanuni na kwamba imepokea, kupitia na hatimae imeridhika na Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mwaka 2022/2023 kwa Wizara ya elimu na mafunzo ya amali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa utekelezaji wa hoja mbali mbali kwa ufanisi. Kamati itaendelea kushauri na kutoa maelekezo ya hoja ambazo utekelezaji wake ulikuwa na mapungufu. Hotuba hii inaunga mkono utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa vile imejitahidi kwa kiasi kikubwa katika utekelekezaji wa majukumu hayo licha ya changamoto ndogo ndogo ambazo kimsingi utatuzi wake unaendelea kufanyiwa kazi. Hata hivyo, Kamati inapongeza Serikali kwa ujumla kwa kukamilisha miradi yote ya ujenzi wa skuli mpya kwa Unguja na Pemba.

CHUO KIKUU CHA TAIFA (SUZA)

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuwawezesha SUZA kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji waliyonayo na kupata vibali vyengine vya kuajiri wanataaluma waliostaafu ambao bado wana uwezo wa kuendelea na kazi za kufundisha, kuajiri wanataaluma kutoka nchi za nje na kutoa kibali cha kuomba uhamisho wa watumishi wanaokidhi vigezo kutoka sehemu mbali mbali ili kufidia nafasi zilizoachwa na wanataaluma waliopata uhamisho na uteuzi.

Sambamba na hilo**,** Kamati ilishauri kuongezwa Bajeti ya mishahara ya chuo kikuu cha Taifa (SUZA). Hivyo Kamati imeridhika na utekelezaji wa suala hili. Chuo kimeweza kupata nyongeza kwa viwango tofauti kwa mujibu wa taaluma zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inapongeza kutengwa Bajeti ya Maendeleo ili kujenga miundo mbinu mipya pamoja na kufanya ukarabati mkubwa wa Majengo katika Kampasi zote zinazosimamiwa na SUZA. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuzingatia kuwepo bajeti ya ukarabati ili kuwa na miradi bora na endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshauri kuwa licha ya Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar kutenga Bajeti maalum ya Chuo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa katika Maabara ili kutoa wahitimu waliobobea katika fani zinazohitajika kwa maendeleo endelevu ya Taifa hili, Kamati inapendekeza kuwepo mpango endelevu wa ununuzi wa vifaa hivyo kupitia makusanyo ya ndani na miradi mbali mbali ya Chuo.

SKULI YA SAYANSI YA BENJAMIN WILLIAM MKAPA TAWI LA SUZA PEMBA

Mheshimiwa Spika, Katika kulipatia ufumbuzi suala la udhibiti wa eneo, Kamati inashauri kuzingatiwa suala la muda katika utekelezaji wa agizo la ujenzi wa uzio katika Skuli ya Sayansi ya Benjamin Mkapa ili kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia kwavile changamoto hiyo ni ya muda mrefu ambayo inaweza kuleta athari mbali mbali ikiwemo eneo hilo kuvamiwa .

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza SUZA kwa kutekeleza Agizo la Serikali kuwatumia Wakala wa ulinzi JKU na kufunga nao Mkataba kwa shughuli za ulinzi katika Kampasi hiyo. Sambamba na kuimarisha suala la usafi katika Kampasi ya chuo kwa kuzitumia kampuni maalum za usafi na kwa maeneo ambayo kampuni hawayafikii hutumika wanafunzi wa chuo kuimarisha usafi huo.

SKULI YA AFYA NA SAYANSI YA TIBA

Mheshimiwa Spika, Ingawa jitihada mbali mbali zimefanyika katika kulitafutia ufumbuzi tatizo la muda mrefu la miundombinu ya maji safi na salama katika Dakhalia za wanafunzi**,** Kamati inaiomba Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuharakisha kusaidia katika upatikanaji wa maji safi na salama ya uhakika katika eneo hilo, maji yanayotumika hivi sasa ni ya chumvi ambayo yanaweza kuhatarisha afya za wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu suala la Ajira za walimu katika Taasisi hii, Kamati imeshauri Wizara kuajiri walimu wenye sifa pamoja na kusomesha wataalamu katika fani ya Afya ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wataalam iliyopo katika Fani hiyo. Ipo haja kwa Serikali kuwa na Mpango wa muda mrefu wa kuwa na wataalum hasa kutoka ndani katika kada ya Afya.

Aidha, Kamati inaishauri wizara katika mpango wake wa ujenzi wa uzio katika skuli hiyo kuanza hatua ya awali na uzio wa nguzo kwa mujibu wa fedha zilizopo.

SKULI YA BIASHARA CHWAKA

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa hoja ya kuwepo kwa changamoto ya muda mrefu ya Usafiri, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika ununuzi wa magari

kwa Taasisi zinazokabiliwa na changamoto kubwa ya usafiri. Kamati imebaini kuwa Kurugenzi nyingi za Wizara pamoja na Dahalia za Vyuo zimekua hazina usafiri unaoridhisha hali inayopelekea usumbufu kwa walimu, wanafunzi na hata kuzorota utekelezaji wa shughuli za Wizara.

SKULI YA KOMPYUTA, MAWASILIANO NA MAFUNZO HABARI ZANZIBAR

Mheshimiwa Spika, Kamati inakipongeza Chuo Kikuu cha Taifa suza kwa kutenga fedha kwa ajili ya Mradi wa ujenzi wa Majengo ya Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari katika eneo walilopatiwa na Serikali kama ilivyoelekeza na Kamati.

Aidha, Kamati imeridhika na hatua nzuri ya kuzingatiwa suala la ukarabati wa majengo ya Skuli ya Kilimani yanayotumika hivi sasa kwa kuwekewa Bajeti ya shilingi Milioni 45 kutoka katika makusanyo ya ndani pamoja na suala la uajiri wa kada zinazohitajika katika Skuli hiyo ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari.

IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Mheshimiwa Spika, Kamati ilieelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, Skuli hiyo ilipokea kiasi cha shilingi Milioni 100 kwa ununuzi wa vifaa katika fani ya Umeme, Makanika na Useremala. Hata hivyo Kamati imeona kuwa bado utekelezaji wa suala hili hauko vizuri sambamba na mazingira ya Dahalia za wanafunzi wanawake na wanaume. Kamati inaishauri Wizara kwavile imetenga tena Bajeti ya ununuzi wa vifaa katika mwaka wa fedha 2023/24 kuhakikisha kuwa suala hilo linatekelezwa vizuri kwa mujibu wa fedha zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuhakikisha kuwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia imeweka utaratibu maalum kwa wanafunzi wanaotoka Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuweza kuendelea na masomo katika Taasisi hiyo kwa kuwapunguzia gharama za malipo ili wanafunzi waweze kuendelea na masomo yao ya Sayansi ambapo wanafunzi 117 waliomaliza Kidatu cha nne mwaka 2022 kutoka Skuli za Mikunguni na Kengeja wanatarajiwa kujiunga na Taasisi ya Karume kwa udhamini wa Wizara.

CHUO CHA KIISLAM PEMBA

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara licha kuwa ipo katika hatua za kurekebisha Mtaala wa vyuo vya Ualimu ili kwenda sambasamba na mahitaji ya mabadiliko ya mifumo ya elimu nchini, ni vyema kuharakisha kukamilisha mchakato huo kwa wakati ili kuweza kuwa na Sheria kamili ya Mtaaala Mpya wa Vyuo vya Ualimu nchini.

OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ustawi wa jamii inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga Bajeti kwa ajili ya kutekeleza ushauri wa Kamati wa Ujenzi wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu pamoja na ofisi za wakaguzi wa Mikoa Unguja na Pemba.

Hata hivyo, Kamati inashauri Wizara kutoa kipaumbele katika suala la ukaguzi wa elimu kwa kuandaa miundombinu bora ya usafiri ili kazi hiyo muhimu ya ukaguzi wa elimu iweze kufanyika kwa mafanikio.

BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuwa na Mpango mzuri wa mabadiliko ya mageuzi ya elimu, Kamati inaishauri Wizara kukamilisha Mchakato wa mageuzi ya Sera ya Elimu ili iweze kurekebisha Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara licha ya kuunda Kamati maalum ya Kitaalamu kufuatilia utekelezaji wa Mikataba ya miradi ya ujenzi, Kamati imebaini kuwa bado Serikali ina mapungufu ya wataalamu katika maeneo mbali mbali ya usimamizi wa Miradi ya maendeleo, ikiwemo Miradi ya Ujenzi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hivyo Kamati inashauri kuajiri wataalam wa kutosha katika eneo hilo.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuwaajiri na kuwatumia ipasavyo Wataaalamu Elekezi katika utekelezaji wa Miradi ya maendeleo ili kuepusha changamoto ya upotevu wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeridhika na utekelezaji wa Wizara kupitia Bodi yake ya Mikopo, kuweka mkazo katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wetu kujiunga na masomo ya fani mbali mbali ikiwemo fani za Uchumi wa Buluu katika vyuo vya kitaaluma. Hata hivyo Kamati inahimiza kuanzishwa Vyuo vya Ubaharia na kutolewa Udhamini wa Mikopo kwa Wanafunzi waweze kujiunga katika vyuo hivyo ili kuenda sambamba na Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu.

HITIMISHO

Mheshiiwa Spika, Kwa kumalizia Hotuba yangu Kamati inaiomba Wizara kuendelea kushirikiana na Kamati ili kufanikisha vizuri majukumu tuliyopewa na Baraza letu tukufu.

Mheshimiwa Spika, Mwisho kabisa, naomba kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa mashirikiano yao waliyonipa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi hii na kwa ruhsa yako naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani Mwenyekiti
2. Mhe. Nassor Salim Ali Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Hussein Kombo Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis Mjumbe
5. Mhe. Haji Omar Kheir Mjumbe
6. Mhe. Panya Ali Abdalla Mjumbe
7. Ndg. Salha Adulla Abdulla Katibu
8. Ndg. Talib Enzi Talib Katibu

Mheshimiwa Spika, Nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa. Naomba waheshimiwa wajadili utekelezaji wa maoni ya Kamati na kutoa maelekezo na ushauri zaidi ili kuleta ufanisi katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Sabiha Filfil Thani

Mwenyekiti,

Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.